# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA TANO

**04 NOVEMBA, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

___________________

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA TANO – TAREHE 04 NOVEMBA, 2024

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**68. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUWAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali haioni haja ya kutenga walau asilimia 5 kwa kila Mradi wa Kisekta ili kuwagusa Vijana.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**69. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaigawa Kata ya Mwangeza kuwa Kata za Ikulu, Mwangeza na Dominila na Vitongoji vya Midimbwi, Nyeri na Mulumba kuwa Vijiji.

**70. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya Kata za Lwamgasa, Nyakagomba na Magenge - Busanda.

**71. MHESHIMIWA CHARLES JOHN MWIJAGE (MULEBA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara ya Kata ya Rutoro itajengwa kwani maombi yalishawasilishwa TARURA.

**OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

**72. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, ni miradi mingapi ya kimkakati imetekelezwa katika Wilaya ya Tunduru.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**73. MHESHIMIWA RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN (CHAKECHAKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini tathmini ya athari za kimazingira zitokanazo na Maji ya Bahari kwenye mashamba ya Mpunga - Bonde la Tibirinzi Chakechake itafanyika.

**WIZARA YA NISHATI:**

**74. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la kukatika kwa Umeme Wilaya ya Meatu.

**WIZARA YA FEDHA:**

**75. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, nini mpango wa kuwalipa Wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali hususani chakula kwenye Shule za Serikali wanaodai kwa muda mrefu.

**76. MHESHIMIWA SALUM MOHAMMED SHAAFI (CHONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Akaunti ya Fedha ya Pamoja ya Muungano imeshafunguliwa.

**WIZARA YA AFYA:**

**77. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):**

Je, Serikali haioni haja kuhuisha Taasisi ya Lishe badala ya kuifuta kabisa.

**WIZARA YA UJENZI:**

**78. MHESHIMIWA SAMWELI XADAY HHAYUMA (HANANG'):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Bashnet – Luqmanda – Bosedesh hadi Zinga itapandishwa hadhi kutoka TARURA kwenda TANROADS.

**79. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, nini mpango wa Serikali kupanua na kuboresha Barabara ya Nangurukuru hadi Kilwa Masoko.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**80. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege Kahama ili uwe na hadhi ya kutua Ndege kubwa.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**81. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, ni Mtaala gani unafundishwa kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Tanzania.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**82. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itakarabati na kujenga Nyumba za Askari Polisi Mkoani Mbeya.

## WIZARA YA MAJI:

**83. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa Miradi ya Maji ya Ziwa Victoria katika Kata ya Igoweko, Uswaya na Tambalale - Manonga.

## WIZARA YA KILIMO:

**84. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga Soko la kuuzia zao la Muhogo katika Mkoa wa Kigoma.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**85. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mkakati gani wa kuwaongezea bajeti TANAPA na TAWA kwani majukumu yao ni makubwa ikilinganishwa na bajeti inayotengwa.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**86. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itaanzisha Maabara ya kupima Sampuli za Magonjwa ya Mifugo Mkoani Kagera.

**87. MHESHIMIWA MARIAM MADALU NYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Wavuvi wameshirikishwaje katika mpango wa Serikali wa ununuzi wa Boti za Uvuvi.

## III. KAMATI YA MIPANGO:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **04 NOVEMBA, 2024** | **KATIBU WA BUNGE** |